

Sura Mbaya ya Siasa katika Demokrasia (Imetafsiriwa)

Habari:

Mkutano Mkuu wa UMNO (United Malay National Organization) uliomalizika mnamo tarehe 11 Juni 2023, umeandika historia nyingine kuhusu hali ya kisiasa ya kidemokrasia ya nchi hiyo kwa uwepo wa viongozi wa chama cha Democratic Action Party (DAP) kwenye hafla hiyo. DAP kwa muda mrefu imekuwa adui mkuu wa kisiasa wa UMNO na ina mawazo ambayo yanapingana nayo kikamilifu. UMNO hupigania marupurupu ya mbio za Malay huku DAP ikipigania usawa wa jamii zote ingawa chama hicho kinatawaliwa na Wachina. DAP pia inaonekana kuwa inapinga vikali juhudi zozote za kuifanya Malaysia kuwa nchi ya Kiislamu. UMNO kwa muda mrefu imekataa uhusiano wowote na DAP, lakini baada ya uchaguzi mkuu wa 15, vyama vyote viliposhindwa kupata kura nyingi ili kuunda serikali, kila kitu kilibadilika.

Maoni:

Kugawanya madaraka miongoni mwa vyama vya kisiasa vyenye mitazamo tofauti hutokea takriban katika nchi zote zinazotekeleza siasa za kidemokrasia. Hili linapotokea, tofauti za kanuni na kifikra hazifai tena. Cha muhimu ni kupata na kubaki madarakani. Hii ni dhana iitwayo uhalisia wa mambo (pragmatism) ndani ya utekelezaji siasa za kidemokrasia. Katika demokrasia, kigezo cha kubaini ukweli wa wazo au kitendo ni manufaa yanayoletwa na wazo/kitendo. Fikra ya Pragmatism katika siasa za kidemokrasia inaweza kueleweka kutokana na maneno ya Lord Palmerson, Waziri Mkuu wa zamani wa Uingereza katika karne ya 19 ambaye alisema; "Hatuna marafiki wala maadui wa kudumu. Maslahi yetu pekee ndiyo yanayobaki na tunapaswa kuyafuata." Alichomaanisha kinaweza kuzingatiwa kwa urahisi leo. Vyama vilivyokuwa maadui, sasa vimekuwa 'marafiki' na vinaweza kukaa meza moja, kugawanya madaraka serikalini. Wanapuuza kanuni zao zinazokinzana kwa njia ya maridhiano ili kufikia manufaa ya pamoja ya mamlaka. Katika siasa za pragmatiki za demokrasia, dhati ya ukweli hakina thamani. Yote yaliyopo ni sura ya kisani yanayotokana na nadharia ya Machiavelli - lengo huhalalisha njia. Ikiwa hakuna ukweli halisi, basi hakuna hatua thabiti za kisiasa. Matendo ya vyama vya kisiasa vya leo yanaendeshwa tu na madaraka na ufikiaji wa maslahi. Ukweli umekuwa hauna maana tena.

Uislamu unafundisha kwamba imani ya kweli (imani) inaweza kupatikana tu kupitia kufikiri kimantiki. Kwa kufikiri kimantiki, tunapata kwamba nyuma ya ulimwengu, uhai na mwanadamu, kuna Muumba Mkuu, Mwenyezi Mungu (swt). Mwenyezi Mungu (swt) ameiteremsha Qur'an kupitia Mtume wake (saw) ili kutoa muongozo kwa mwanadamu katika nyanja zote za maisha ikiwemo siasa. Imani juu ya Mwenyezi Mungu (swt), Qur'an na Mtume Wake (saw) inaruhusu kila Muislamu kuelewa uhusiano wake Naye katika kila wakati katika maisha yake. Ingawa Imani, mwanadamu atatenda kulingana na maamrishi na makatazo ya Mwenyezi Mungu (swt). Shari'a ya Uislamu ni kigezo na kipimo cha haki; manufaa kama lengo la kitendo hayana nafasi katika Uislamu. Kwa hivyo, kwa kushikamana na Shari'a, fikra na matendo ya mwanadamu yatakuwa sawa daima. Katika kupata nguvu kwa mfano, Mtume (saw) alitonyesha sisi kushikamana kwa uthabiti na tariqa (njia) na kutolegeza msimamo na mambo yanayokengeuka kutokana nayo. Hiyo ndiyo da'wah ya Kiislamu na siasa zilizoonyeshwa na Mtume (saw). Hakuna mikengeuko au kurudi nyuma kama katika siasa za demokrasia.

Siasa za demokrasia zinasimama kwa misingi ya manufaa na maslahi. Hazisimami kwenye ukweli. Vyama vya kisiasa vya kidemokrasia, kiasili, husimama kwenye dhana ya upragmatiki na maridhiano. Harakati zote za kisiasa za kidemokrasia, hata zile zinazoitwa za 'Kiislamu' zinaendeshwa kwa misingi hii. Wale wanaojaribu kutembea kwenye njia tofauti watakuwa na kila kitu cha kupoteza, kudhalilishwa na kuachwa nyuma. Hali hii kamwe haitabadilika isipokuwa juhudi zifanywe kung'oa mfumo wa kidemokrasia kupitia mapinduzi ya kifikra na kusimamisha mfumo wa kweli wa kisiasa wa Kiislamu juu ya mavumbi ya uharibifu wa siasa za kisekula za kipragmatiki za kidemokrasia.

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na
Dkt. Mohammad – Malaysia**